

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

عَوَاقِبُ تَرْكِ الصَّلَاةِ وَالْإِسْتِخْفَافِ بِهَا

ADHABU ZA (MTU MWENYE) KUACHA SALA NA KUIPUUZA.

Siku moja Bibi Fatwimatu-z-Zahra (a.s) alimuuliza babaye Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba:-	سَأَلَتْ فَاطِمَةَ الزَّهْرَاءُ - أَبَاهَا رَسُولَ اللَّهِ
Ewe Baba yangu, Ni adhabu ipi anayoipata mwenye kuacha sala (na kuipuuza) katika wanaume au wanawake?	يَا أَبَتَاهُ! مَا لِمَنْ تَهَاوَنَ (أَيِ اسْتَخَفَّ) بِصَلَاتِهِ مِنَ الرِّجَالِ وَ النِّسَاءِ؟
"Akasema Mtume Muhammad (s.a.w.w) kumjibu mwanae Fatwimah (a.s) kwamba:- Mwenye kuiacha swala na kuipuuza katika wanaume na wanawake basi Mwenyezi Mungu humpa mitihani (adhabu) 15:	فَقَالَ (ص): "فَمَنْ تَهَاوَنَ مِنَ الرِّجَالِ وَ النِّسَاءِ ابْتَلَاهُ اللَّهُ بِخَمْسَ عَشْرَةَ خَصْلَةً:
(ambapo katika adhabu hizo 15 sita miongoni mwazo atazipata hapa duniani na adhabu 3 atazipata katika nguvu zake na adhabu 3 ndani ya kaburi lake hali kadhalika adhabu 3 atazipata siku ya Qiyamah pindi atakapofufuliwa katika kaburi lake!!)	
Ama adhabu ambazo atakazozipata duniani ni kama zifuatazo:-	• أَمَّا اللّٰوَاتِي تُصِيبُهُ فِي دَارِ الدُّنْيَا :
1. Mwenyezi Mungu huziondoa baraka zake katika umri wake (wote).	1 - يَرْفَعُ اللَّهُ الْبَرَكَاتِ مِنْ عَمْرِهِ
2. Vile vile Mwenyezi Mungu huondoa baraka katika riziki yake (ambazo huzichuma).	2 - وَ يَرْفَعُ اللَّهُ الْبَرَكَاتِ مِنْ رِزْقِهِ
3. Mwenyezi Mungu pia hufuta alama za watu wema katika uso wa mtu huyo (anaepuuza sala).	3 - وَ يَمْحُو اللَّهُ سِيْمَاءَ الصَّالِحِينَ مِنْ وَجْهِهِ
4. Kila kazi aifanyayo (mtu huyo Mwenyezi Mungu) hampatii ujira.	4 - كُلُّ عَمَلٍ يَعْْمَلُ لَا يَأْجُرُهُ عَلَيْهِ
5. Pia dua ya mtu huyo haipandi mbinguni (mbele ya Allah (s.w.t))	5 - وَ لَا يَرْتَفِعُ دُعَاؤُهُ إِلَى السَّمَاءِ
6. Pia mtu huyo hana hadhi (fungu) katika dua ya watu wema (mitume).	6 - لَيْسَ لَهُ حِطٌّ (نُصِيبُ) فِي دُعَاءِ الصَّالِحِينَ
• Ama yale ambayo yatakayompata katika nguvu zake ...!	• - وَ أَمَّا اللّٰوَاتِي تُصِيبُهُ عِنْدَ قُوَّتِهِ :
1. Jambo la kwanza ni kuwa mtu huyo hufa hali ya kuwa ni dhalili (mno).	1 - فَأَوْلَهُنَّ يَمُوتُ ذَلِيلًا
2. Na jambo la pili hufa hali ya kuwa ni mwenye njaa (kali sana).	2 - وَ التَّانِيَةَ أَنَّهُ يَمُوتُ جَائِعًا

3. Na jambo la tatu hufa hali ya kuwa ana kiu (kikali mno)	3 - وَ الثَّالِثَةُ أَنَّهُ يَمُوتُ عَطْشَانًا
Basi hata kama angelinyweshwa maji ya mito ya duniani yote yasingeliweza kuikata kiu yake.	فَلَوْ سَقِيَ مِنْ أَنْهَارِ الدُّنْيَا لَمْ يَرَوْ عَطْشَهُ
• Ama yale ambayo yatakayompata ndani ya kaburi lake	• - أَمَّا اللّٰوَاتِي تُصِيبُهُ فِي قَبْرِهِ
1. Jambo la kwanza: Mwenyezi Mungu humtumia malaika atakayemsumbua kaburini mwake (na kumpa kila aina ya adhabu).	1 - فَأَوْلَهُنَّ يُوَكَّلُ اللَّهُ بِهِ مَلَكًا يَزْعَجُهُ فِي قَبْرِهِ
2. Na jambo la pili ni kuwa hubanwa ndani ya kaburi lake (hadi mbavuze kupishana).	2 - وَ الثَّانِيَةَ يُضَيِّقُ عَلَيْهِ فِي قَبْرِهِ
3. Na jambo la tatu kunakuwa giza totoro (kali / nene) ndani ya kaburi lake.	3 - يَكُونُ الظُّلْمَةَ فِي قَبْرِهِ
• Na ama yatayomsibu siku ya Qiyamah (ni kuwa):	• - وَ أَمَّا اللّٰوَاتِي تُصِيبُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
1. Kwanza, Mwenyezi Mungu atamtumia malaika wa kumkokota uso wake na hadhira (halaiki) ya watu wakimuangalia. (mtu huyo kukokotwa kwa minyororo ya moto katika uso wake kuelekea motoni).	1 - فَأَوْلَهُنَّ أَنْ يُوَكَّلَ اللَّهُ مَلَكًا يَسْحَبُ عَلَى وَجْهِهِ وَالْخَلَائِقُ يَنْظُرُونَ إِلَيْهِ
2. Na jambo la pili huhesabiwa mtu huyo hesabu kali sana.	2 - وَ الثَّانِيَةَ يُحَاسِبُ حِسَابًا شَدِيدًا
3. Ama jambo la mwisho la tatu analolipata mtu huyo mwenye kuipuuza na kuiacha sala yake, ni Mwenyezi Mungu hatomuangalia kwa jicho la huruma siku ya Qiyamah wala kumtakasa, na pia atapata adhabu (kali) iumizayo (mbele ya Allah (s.w.t)).	3 - وَ الثَّالِثَةَ لَا يَنْظُرُ اللَّهُ إِلَيْهِ وَلَا يُزَكِّيهِ وَ لَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ
<p>Mwenyezi Mungu atujalie kuzihifadhi sala zetu Insha-Allah na iwe ni sababu ya kuingia peponi kwa rehema zake. AMIN! AMIN! AMIN!</p>	

Imetafsiriwa na kuandaliwa na :
Sheikh Abdul Rashad Ibrahim.

Imehaririwa na kupangwa kwenye kompyuta na Jamaal A. Kasole Tel: +254 724 124 597 E-mail: jakabul@yahoo.com